

BOARD OF TRUSTEES

WARD A Sherri O'Keefe
WARD B Marsha Nelson
WARD C Marcia Hole
WARD D Trisha Estabrooks
WARD E Dawn Hancock
WARD F Julie Kusiek
WARD G Saadiq Sumar
WARD H Nathan Ip
WARD I Jan Sawyer

SUPERINTENDENT OF SCHOOLS

Darrel Robertson

Centre for Education
1 Kingsway NW
Edmonton AB T5H 4G9
T 780-429-8000
F 780-429-8318
E info@epsb.ca

October 24, 2022

Wapendwa wazazi, walezi na familia,

Msimu huu wa mapukutiko, Shule za Umma za Edmonton zinaanza kazi ya kuelewa vyema zaidi uanuai wa wanafunzi tunaowahudumia. Taarifa hii itasaidia kuboresha hatua zetu ili kufanya shule kuwa mahali pazuri na salama kwa wanafunzi wote. Katika wiki zijazo, wanafunzi wa Gredi za 4 hadi 12 watapata fursa ya kushiriki katika **utafiti wa demografia ya wanafunzi**.

Wanafunzi wanaoshiriki watajaza utafiti wakati wa muda wa darasa kwa kuzingatia faragha yao, na wafanyakazi wa shule watakuwepo kuwasaidia wanafunzi inapohitajika. Maswali yote ya utafiti ni ya hiari, ambayo inamaanisha kwamba mtoto wako atajibu tu maswali anayotaka kujibu.

Utafiti wa Demografia ya Wanafunzi ni nini?

Katika msimu wa mapukutiko wa 2021, Shule za Umma za Edmonton zilitoa [Anti-racism and Equity Action Plan](#) (Mpango wa Hatua za Kuleta Usawa na Kupambana na Ubaguzi wa Kimbari) ili kukabiliana na ubaguzi wa kimbari katika Idara na kuchukua hatua za kuleta usawa. Mpango huo unajumuisha maeneo matatu muhimu. Maeneo haya yaliundwa baada ya kusikiliza uzoefu wa wanafunzi, wafanyakazi, familia na [mapendekezo](#) ya Kamati ya Ushauri wa Usawa ya 2020-2021. Mojawapo ya maeneo matatu muhimu yaliyobainishwa katika mpango ni kupata maelezo zaidi kuhusu wanafunzi kwa kukusanya data ya ziada ya kidemografia ili kuboresha hatua zinazoleta mabadiliko chanya.

Kupitia utafiti huu, wanafunzi wataalikwa kushiriki taarifa kuhusu:

- utambulisho wa Asili
- utambulisho wa mbari
- ukabila
- uhusiano wa dini au kiroho
- utambulisho wa jinsia
- mwelekeo wa kijinsia (*Gredi za 7-12 pekee*)

Kwa nini Idara inaomba taarifa hii?

Data kutoka kwa utafiti wa demografia ya wanafunzi itatusaidia kuelewa vyema zaidi uanuwai wa wanafunzi. Data itachambuliwa pamoja na data nyingine ambayo tayari inapatikana kwenye Kitengo. Taarifa hizi zitasaidia Shule za Umma za Edmonton kuelewa vyema hali ya vikundi tofauti nya wanafunzi shulenii na kuboresha hatua zinazoweza kuchukuliwa kusaidia kufaulu kwa wanafunzi.

Muhtasari wa matokeo ya awali na mitindo kutoka kwa utafiti wa demografia utashirikiwa na jamii. Taarifa hii haitatambua shule au wanafunzi binafsi.

Faragha na usalama wa taarifa za mtoto wako

Taarifa za mwanafunzi ni nyeti na ni siri. Kama wasimamizi wazuri wa taarifa, Shule za Umma za Edmonton hufuata *Freedom of Information and Protection of Privacy Act* (FOIP), (Sheria ya Uhuru wa Taarifa na Ulinzi wa Faragha), na mbinu bora za ukusanyaji, uhifadhi na ulinzi wa taarifa na data ya wanafunzi.

Nani ataona majibu ya wanafunzi?

Majibu ya mwanafunzi binafsi yatahifadhiwa kwa usalama kwenye seva kuu na kufikiwa na idadi ndogo tu ya wafanyakazi wa Idara ambao wana jukumu la usimamizi na faragha ya data. Taarifa ambazo wanafunzi watashiriki zitakuwa siri, kumaanisha kwamba hazitashirikiwa na wafanyakazi wa shule, familia au umma kwa ujumla.

Maswali au wasiwasi wa wazazi

Wazazi ambao hawangependa mtoto wao ashiriki katika utafiti lazima wawasili na shule ya mtoto wao kuhusu hili. Wanaweza kufanya hivi kwa njia ya simu, mazungumzo ya ana kwa ana au kwa maandishi.

Matumaini yetu katika siku zijazo

Shule za Umma za Edmonton zimejitolea kupambana na ubaguzi wa kimbari na kuleta usawa. Fursa ya kupata taarifa zaidi kuhusu utambulisho wa mwanafunzi ni hatua moja muhimu katika kuleta mabadiliko muhimu. Matumaini yetu ni kwamba kuititia utafiti huu tutajifunza kuhusu hatua zinazoweza kuboresha mustakabali ambapo wanafunzi wote wanahisi kukubalika na kufaulu.

Kwa dhati,



Darrel Robertson
Msimamizi wa Shule

Taarifa za kibinafsi zinakusanywa kwa mujibu wa Kifungu cha 33(c) cha *Freedom of Information and Protection of Privacy Act* (FOIP), (Sheria ya Uhuru wa Taarifa na Ulinzi wa Faragha) na Sheria ya Elimu ili kusaidia kuunda mazingira mazuri, yanayojali, salama na yenye heshima kwa wanafunzi, wafanyakazi na umma kwa ujumla. Maswali yoyote yanayohusiana na FOIP yanaweza kutumwa kwa Brenda Hoang, Division FOIP Office, Technology and Information Management, The Centre for Education, One Kingsway Avenue, Edmonton, Alberta, Kanada. Simu: +1 780-429-8350.

